*Toleo 93 - Rabi' al-awwal 1446 H / Octoba 2024 M*

# Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Hizb ut Tahrir / Tanzania Inalaani Kutekwa Nyara na Kuuwawa Muhammad Ali Kibao

**MAKALA**
Kusimamishwa kwa Khilafah Rashidah na Dori Yetu

**HABARI NA MAONI**
Je, Tunapaswa Kuzingatia Maneno Yako Mazuri au Matendo Yako Mabaya!

**MATOLEO**
Serikali ya Uswidi Yawataka Waislamu Waachane na Uislamu!



# Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

## Kitengo cha Wanawake
## “Kongamano la Kimataifa la Wanawake: Ukombozi wa Palestina... Changamoto na Bishara Njema”




Mwaka mzima umepita tangu kuanza kwa Kimbunga cha Al-Aqsa na vita vikali vilivyofuata huko Gaza. Tangu tarehe 7 Oktoba mwaka jana, watu wa Gaza wamevumilia mitihani mikubwa, wakiishi katika machungu, mateso, na majanga yasiyohesabika: kuhamishwa, mauaji, njaa... mabaki yaliyotawanyika ya watoto na wanawake yaliyokusanywa kwenye mifuko, na mashahidi walionaswa chini ya vifusi, wasiowezekani kutolewa, na kuongeza katika maumivu na huzuni kutokana na kushindwa kuwaheshimu na kuwazika. Mauaji ya kikatili ya halaiki yanafanywa na umbile halifu kwa mtazamo kamili wa ulimwengu ambao unashiriki na kupuuza. Hata hivyo, licha ya mikasa na majonzi ya vita hivi, vimejaa mafunzo na tafakari zinazotolewa na kundi aminifu, vumilivu na thabiti linalosimama kidete dhidi ya njama za maadui na khiyana za watawala na wale wanaodai kuwa marafiki. Kundi hili dogo, bila kukatishwa tamaa na wale waliowatelekeza, linabaki stahimilivu, bila kupoteza kamwe tumaini la ushindi wa Mola wa mbingu na ardhi. Licha ya vilio, maombi, na wito wa kuomba msaada kutoka kwa watu wa Gaza, majibu yamefichua na kudhihirisha usaliti wa watawala wa Waislamu ambao wamekaa kwenye viti vyao vya utawala, viziwi, mabubu na vipofu kwa uhalifu wa kivita na mauaji ya halaiki yanayofanywa na umbile hilo halifu dhidi ya watu wa Gaza na Palestina kwa jumla. Watawala hawa wamejitolea kuonyesha uaminifu na utiifu kwake, kuhalalisha mahusiano nalo, na kuimarisha uwepo wake.

Vita hivyo pia vimewafichua sura za wanazuoni wengi, na kuwafichua wakweli kutoka kwa wadanganyifu. Vimefunua pazia machoni, vikionyesha ukweli wa kile kinachotokea. Asili ya halisi ya mzozo wa Palestina imekuwa wazi: mapambano kati ya haki na batili, kati ya Waislamu wa Palestina na umbile la Kiyahudi linalokalia kwa mabavu, nyakuzi, la kikafiri. Ndiyo, watu wa Palestina kwa jumla, na hasa Gaza, wameuita Ummah. Hivyo, je jibu lilikuwaje?! Lilikuwa dhaifu, likidhihirika katika maandamano machache, au kususia baadhi ya taasisi na maduka yanayounga mkono umbile hilo, au kutuma chakula na nguo kama msaada! Licha ya umbile hilo vamizi kuendelea kutekeleza uhalifu wa kivita mmoja baada ya mwingine, na licha ya maombi yote hayo yanayokaririwa, vilio vya kuomba msaada, na matukio ya kuhuzunisha, kimya cha dunia nzima, usaliti wa serikali, kimya cha Umma wa Kiislamu na majeshi yake, na ukosefu wao wa kuchukua hatua yamekuwa, na bado yangali, kama majibu yao!

***Endelea... UK 3***

Haya yote yanazua maswali kuhusu sababu za kuzuia kumalizika kwa mauaji haya ya halaiki na ukombozi wa Palestina! Je, ni suluhisho gani la msingi ambalo kwalo kadhia hii inaweza kutatuliwa milele? Maswali haya na mengine yatashughulikiwa na kujibiwa mnamo Jumamosi, Oktoba 5, 2024, wakati wa kongamano la kimataifa la wanawake la mtandaoni lililoandaliwa na Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir, kwa uratibu na wanawake wa Hizb ut Tahrir kote duniani, chini ya kichwa: “Ukombozi wa Palestina: Changamoto na Bishara Njema” Kongamano hili litaainisha njia sahihi ya kutatua kadhia hii na mambo mengine yanayohusu Umma wa Kiislamu. Litaangazia nukta muhimu za kadhia ya Palestina na kutoa suluhu zinazohitajika ili kukomesha mateso ya watu wa Palestina na Waislamu kwa jumla, kwa kuzingatia kuwa ni kadhia ya Ummah mzima na sio kadhia ya kitaifa inayofungamana na mipaka bandia iliyoundwa na dola za kikoloni. Wazungumzaji kutoka Palestina, Tunisia, Syria, Lebanon, Indonesia, na Amerika watashiriki. Kongamano hili litawafichua wale wanaozuia kumalizika kwa mauaji hayo ya halaiki, kufafanua sababu za kuzuia kukombolewa Palestina kutoka kwa Mayahudi, na kujadili dori ya taasisi za kimataifa na maamuzi yao katika kula jama dhidi ya kadhia ya Palestina. Zaidi ya hayo, litazungumzia dori ovu ya vyombo vya habari katika kupotosha na kuficha ukweli, na kuionyesha kama ni kadhia ya kitaifa au ya kikabila, ili kuwapotosha Waislamu kutoka kwenye njia sahihi ambayo wanapaswa kufuata ili kuitatua kimsingi.

Kongamano hili pia litazungumzia dori ya Umma wa Kiislamu katika kufikia suluhisho hili la kimsingi, ambalo lazima litoke kwenye Aqida (itikadi yake). Litaangazia kwamba masuluhisho yaliyopandikizwa na maadui na wakoloni ni silaha tu zinazotumiwa kuupiga vita Ummah, kuupotosha kutoka kwenye njia sahihi. Masuluhisho ya kivipande na ya muda yanayopendekezwa si chochote zaidi ya njia ya kuutia ganzi Ummah, kuuzuia kuchukua dori ambayo lazima uicheze. Kongamano hilo pia litaelezea vikwazo vinavyowazuia watu kutabanni ruwaza ya Kisharia kwa ajili ya ukombozi wa Palestina, na litafafanua kwa nini majeshi yanasalia katika kambi zao, kutoitikia wito wa mara kwa mara wa kuchukua hatua.

Zaidi ya hayo, kongamano hilo litafichua juhudi zinazolenga kupanua mwanya kati ya Ummah na majeshi yake kwa kuyaonyesha majeshi hayo kuwa hayana nguvu, tiifu kwa tawala, na hayana uwezo wa kutoa nusra au ushindi. Madai na tuhma hizi zitakanushwa kwa kutoa mifano ya watu wenye ikhlasi ndani ya jeshi waliojitolea mhanga kwa ajili ya dini yao na ushindi wake, na kubainisha dori ya ufahamu na rai jumla katika kuwahamasisha watu wengi wenye ikhlasi katika majeshi kuchukua hatua.

Aidha, kongamano hilo litafichua sababu msingi zilizo nyuma ya kuweka mzigo wa kukomboa ardhi takatifu kwa watu wa Palestina pekee, huku zikificha mjadala kuhusu dori ya Umma na majeshi yake, ambayo yana vifaa vya kutosha na yako tayari.

Kongamano hilo pia litaangazia dori ya kila Muislamu katika kutatua kadhia hii, kwa kuzingatia makhsusi wanawake wa Kiislamu na hatua wanazopaswa kuchukua ili kuchangia kukomesha mauaji ya halaiki na uchinjaji unaofanywa dhidi ya watu wetu wa Gaza na Palestina kwa jumla. Litasisitiza wajibu wao wa kufanya kazi pamoja na wengine wanaopigania ukombozi wake. Kongamano hilo litasisitiza ahadi ya Mwenyezi Mungu ya ushindi na tamkini, na kutukumbusha kwamba faraja huja baada ya dhiki, na kwamba ushindi hufuata mitihani. Litasisitiza tena utukufu wa Ummah huu, wenye uwezo wa kupata ushindi Inshallah.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) kwamba kongamano hili litaangaza njia sahihi ambayo Ummah unapaswa kuchukua ili kuregesha tena mamlaka yake, uongozi, na kufikia ukombozi wa Palestina kutoka mikononi mwa maadui na makafari. Kama anavyosema Mwenyezi Mungu:

وَلَيَنْصُرَنَّ اللهُ مَنْ يَنْصُرُهُ إِنَّ اللهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ

**“Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu.”** [Al-Hajj:40].

**Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Jumatano, 22 Rabi’ ul-Awwal 1446 H sawia na 25 Septemba 2024 M**

Afisi ya Habari Tanzania

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 03/1446 Jumanne, 07 Rabi'I 1446 H 10/09/2024 M

**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Hizb ut Tahrir / Tanzania Inalaani Kutekwa Nyara na Kuuwawa Muhammad Ali Kibao

Hizb ut Tahrir / Tanzania inatoa mkono wa pole na kuifariji familia na jamaa kufuatia kuuwawa kada wa Chadema Muhammad Ali Kibao ambaye alitekwa nyara mnamo Septemba 6, 2024 na kisha kuuwawa.

Tunalaani vikali utekaji nyara huo na mauaji hayo ya kikatili, kisha tungependa kutamka yafuatayo:

1. Vitendo vya utekaji nyara vinavyopelekea kupotezwa au kuuliwa kikatili si vigeni Tanzania, vimekuwapo kwa muda sasa, ambapo wahanga wakubwa wa ukatili huo ni Waislamu kwa Uislamu wao. Kwa mfano, kuna wahanga zaidi ya 380 hawajulikani walipo katika wilaya za Mkuranga, Kibiti na Rufiji kufuatia kamata kamata ya serikali ndani ya mwaka 2017 iliyoambatana na mateso na mauaji ya kiholela' (The East African, May, 2018).

2. Matukio kama haya sio tu yanaleta hofu, ukosefu wa amani, kuchafuka na kuathirika haiba ya serikali, bali pia ni kielelezo cha wazi cha kukosekana uwajibikaji wa serikali, kwa kuwa dola ndio mdhamini mkuu na mlinzi wa usalama wa raia, mali zao na heshima zao.

3. Aidha, matukio kama haya yanaonesha wazi wazi kushindwa kwa mfumo wa kibepari na demokrasia yake ulimwenguni kote, kwa kuwa mfumo huo unazua machafuko, vurugu na utovu wa amani kwa wanadamu.

Ni wazi, ulimwengu unahitaji mfumo wa haki na uadilifu ambao si mwengine bali ni Uislamu. Mfumo huo una uwezo wa kudhamini ulinzi wa raia, maisha, mali na heshima zao.

**Masoud Msellem**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania**

# HABARI NA MAONI
# Je, Tunapaswa Kuzingatia Maneno Yako Mazuri au Matendo Yako Mabaya!




**Habari:**

Katika hotuba yake katika Programu ya Ufunguzi wa Wiki ya Mawlid al-Nabi Rais Erdoğan alisema, "Mtu pekee katika ulimwengu huu ambaye tunamuiga, tunafuata nyayo zake na ambaye tunajitolea maisha yetu kwake ni Mtume wetu wa Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye kiongozi wetu na kipenzi chetu ambaye tutakufa kwa ajili yake. Mola wetu atujaalie tutembee katika nyayo za Mtume wa Mwenyezi Mungu, tujenge shakhsiya yetu kwa maisha yake, na tuwe na maadili mema ya kupigiwa mfano." (Mashirika 14.09.2024)

**Maoni:**

Uovu mkubwa kabisa wanaoweza kuufanya watawala wanaochunga mambo ya watu, ni kuitawala jamii kwa mifumo inayotoka kwenye itikadi ya kisekula ambayo huwaweka watu mbali na Mola wao, ambayo huwafanya watumwa wa matamanio yao kwa udanganyifu wa uhuru na uliberali, na ambayo hutia utumwa kwa mja. Balaa kubwa zaidi kwa Waislamu ni dharau za watawala wanaotulazimishia masuluhisho ya fikra hizi za dhana potofu juu yetu. Rais Erdoğan ambaye ni gwiji wa kuongea kulingana na mapigo ya moyo, amejiwekea sifa ya kuzungumza kulingana na mazingira ya mchakato anaouingia. Kwa kuzingatia kanuni kwamba neno ni amana, ikiwa kiongozi pekee katika maisha yako ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na unadai kufuata nyayo zake, basi vitendo vyako vinapaswa kuthibitisha maneno haya mazuri.

Umakini na taqwa ya watawala wanaobeba mambo ya jamii katika maisha yao binafsi inahusiana na matendo yao na haihusu jamii. Hata hivyo, mifumo ya kikafiri na mawazo ya potofu ambayo yamewekwa kwa jamii itakuwa ni jukumu na lawama ya kila mtu binafsi, na hii ndiyo sehemu inayotuhusu. Katika muktadha huu, unaweza kuzungumza juu ya kufuata kiigizo cha Mtume wa Mwenyezi Mungu kadiri unavyotaka katika maisha yako binafsi, lakini maadamu kuna mfumo wa kidemokrasia wa kisekula wa ukafiri ambao kupitia kwayo unatawala jamii, matendo yako daima yatakinzana na maneno yako. Ubaya na harufu mbaya ya matendo yako itasumbua jamii daima. Tunategemea maneno ya watawala ambao matendo yao yatathibitisha maneno yao, ambao mwanzo watashikilia amana ya neno, ambao hawatausaliti Ummah na utukufu, na ambao wataifanya dini kuwa msingi wa utawala wao. Lakini Rais Erdoğan, kama nilivyotaja hapo juu, anaona ni siasa kuzungumza kulingana na mazingira na wakati, hivyo wakati mwingine anaionyesha Quran Tukufu kwenye viwanja vya uchaguzi. Nyakati nyingine, yeye huchochea umma kwa fasihi ya nchi na taifa. Wakati mwingine anaenda mbali zaidi na kuunadi usekula kwa watu katika sehemu mbalimbali za Jiografia ya Kiislamu kwa niaba ya Marekani. Demokrasia ni neno la kichawi ambalo kamwe halibanduki kwenye ulimi wake!

Bw. Erdoğan! Katika miaka yako 23 ya madaraka, ni hukmu ipi kati ya hukmu za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ambayo umeitekeleza ili useme kwamba unafuata nyayo zake na kwamba umemfanya kuwa kiongozi wako pekee? Je, udanganyifu, uhadaifu na upotoshaji wote uliofanya wakati wa utawala wako hautoshi! Kwa nini unasema mambo ambayo hukuyafanya, ambayo huwezi kuyafanya, kana kwamba umeyafanya, kana kwamba utayafanya, wakati huu ni mzigo mkubwa mbele ya Mwenyezi Mungu (swt)? Lau kweli ungefuata nyayo za Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), ungelikusanya jeshi zima na kukomesha dhulma hii huko Gaza ambayo imekumbwa na mauaji ya halaiki ambayo historia kamwe haijawahi kuyashuhudia mbele ya macho yako kwa muda wa mwaka mmoja. Hatutegemei sentensi za kupumbaza, bali tunategemea maneno ya watawala ambao ni kama watu wanaoyapamba matendo yao kwa hukmu za Uislamu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu (swt) aziangamize nguvu za watawala Ruwaybidha, wanaoutesa Umma wa Kiislamu, na alete siku ambazo Makhalifa Rashid (walioongoka), ambao maneno na matendo yao ni kitu moja, watauongoza Ummah mara tu inawezekana.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ahmet SAPA**

# Kusimamishwa kwa Khilafah Rashidah na Dori Yetu



Kuna mijadala mingi kuhusu kusimamishwa kwa Khilafah siku hizi katika Ulimwengu wa Kiislamu na Magharibi. Kule ambako Khilafah itasimamishwa kwanza, iko Mikononi mwa Mwenyezi Mungu Peke Yake, kwani Yeye Pekee hupeana Nasr (ushindi). Bishara njema za Mtume (saw) zinatoa habari (khabar) juu ya jambo la uwezekano. Ama dori yetu ni kufuata njia ya Utume, kusimamisha Uislamu katika kutawala mambo yetu.

Tangu mtihani wa Gaza ulipoanza, ni dhahiri kwamba Mwenyezi Mungu (swt) anautayarisha ulimwengu kuhusiana na Dini ya Haki. Leo, Ulimwengu mzima wa Kiislamu unazungumza juu ya haja ya kuregea Uislamu, kutabikisha Shariah na kuungana kama Ummah mmoja. Baadhi ya mazungumzo haya yamepanuka hadi kwenye mjadala kuhusu Zama za Mwisho na kurudi kwa Khilafah. Ulimwengu mzima umeathirika pia. Tunaona sauti zinazowaunga mkono Waislamu miongoni mwa watu wenye mawazo ya adilifu katika nchi za Magharibi.

Bishara njema za Mtume (saw) zimesomwa kwa karne nyingi na maulamaa mahiri wasiohesabika. Kama wanafunzi, tunaweza kuona kwamba khabar (habari) hii inawashajiisha Waislamu kufanya matendo mema. Baadhi ya khabar (habari) huja kwa namna ya talab (amri) kutekeleza hukmu maalum, kama vile kupigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Ndiyo, tunaweza kutofautiana katika tafsiri, lakini licha ya tafsiri zetu, ni lazima tushikamane na amri za Kiislamu kuhusu hali yetu.

Kuhusu kile tunachopaswa kufanya, tunaregea kwenye Sira ya Mtume (saw):

a. Mtume (saw) aliwatayarisha jamaa na marafiki zake katika Dar ul Arqam. Nyumba zetu, familia, marafiki na jamii lazima ziwe mifano ya Dar ul Arqam. Ni lazima wawe vinara wa Dini na mwongozo wake wenye nuru, sehemu za kujifunzia na kuutekeleza Uislamu.

b. Mtume (saw) aliitayarisha jamii kwa ajili ya kuhukumu kwa Uislamu. Alizungumzia sheria zinazotawala mahusiano ya watu, kama vile kuamiliana na watoto wachanga wa kike, maskini, mayatima na udanganyifu katika biashara. Katika zama zetu hizi, ni lazima pia tuhutubie jamii, hadharani, tukishughulikia maovu yake na kuupeana Uislamu kama badali. Kwa hakika, Qur'an Tukufu na Sunnah za Mtume zinatoa mwongozo kamili wa uchumi, sera za kigeni, sera ya elimu na utawala.

c. Mtume (saw) pia aliwatayarisha watu wenye uwezo na nguvu ili kunusuru utawala kwa Uislamu. Yeye (saw) aliwaendea wapiganaji wa makabila na akawataka Nusrah (Msaada wao wa Kimada) kwa ajili ya kusimamisha Uislamu. Makabila ya Yathrib yaliitikia vyema, baada ya makabila mengi kukataa. Kupitia Kiapo cha Pili cha utiifu cha Aqabah, Nusrah ilipanuliwa hadi kuhukumu kwa Uislamu. Yathrib ikawa mamlaka ya Kiislamu kwa jina linalopendwa la Al-Madinah Al-Munawwarah, ambalo lilitoa mwanga mkali kwenye Bara Arabu. Kwa hivyo leo, lazima tuwaandae wana wetu, kaka na baba zetu katika jeshi ili kutoa Nusrah yao pia.

Kuhusu wapi tunapaswa kufanya kazi,

a. Inajulikana kuwa baadhi ya maeneo yanakubalika zaidi na mengine kidogo. Makka ndipo mahali ambapo Dawah kwa ujumbe wa Risaalah ya Mtume (saw)

***Endelea... UK 7***

ulitokea kwa mara ya kwanza. Hata hivyo, ilikuwa pizani kwa ujumbe huo, ikihisi kupendelewa na kufaidika na hali halisi ilivyo. Kinyume chake, Yathrib ilikuwa yeye kuupokea, ikikumbana na mitihani na matatizo mengi. Ulimwengu wa Kiislamu ni mahali pazuri pa kufanya kazi. Umejaa Waislamu wanaopenda Uislamu na wanapenda kujifunza kuhusu Uislamu. Umezama katika shida na kutafuta njia ya kujitoa.

b. Sisi tunaoishi katika Ulimwengu wa Kiislamu tuna ndugu na marafiki wengi. Ni mahali pa kimaumbile kwetu kuanza. Lazima sote tujifunze na sote lazima tufunze. Ni lazima sote tushughulikie jamii na kuwasilisha hukmu za Shariah za kutibu maovu yetu ya kijamii. Ni lazima sote tuwasiliane na jamaa na marafiki zetu katika majeshi.

c. Ndiyo, baadhi yetu tumelazimika kuhama nje ya Ulimwengu wa Kiislamu kutokana na matatizo. Hata hivyo, kama Waislamu walioondoka kwenda Abyssinia, nyoyo na matarajio yetu yanabakia kwa Ulimwengu wa Kiislamu. Sote tuna jamaa na marafiki katika Ulimwengu wa Kiislamu. Tunaweza kuanzisha miundo ya kidijitali ya Dar ul Arqam, kujifunza Uislamu na kufikisha Uislamu. Tunaweza hata kutembelea. Na pengine, baada ya Dua na maandalizi, tunaweza hata kutafuta njia ya kurudi.

**Enyi Waislamu!**

Ahmed amesimulia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema,

**ثُمَّ تَكُونُ مُلْكًا جَبْرِيَّةً فَتَكُونُ مَا شَاءَ اللَّهُ أَنْ تَكُونَ ثُمَّ يَرْفَعُهَا إِذَا شَاءَ أَنْ يَرْفَعَهَا ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةً عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ**

“**Kisha kutakuwa na utawala wa kutenza nguvu, na atakuwepo apendapo Mwenyezi Mungu uwepo kisha Mwenyezi Mungu atauondoa apendapo kuuondoa. Na kisha kutakuwa na Khilafah kwa Njia ya Utume.**” Na kisha (saw) akanyamaza. Kauli hii iliyobarikiwa ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw), ambayo si chochote isipokuwa Wahyi uliovuviwa na Mwenyezi Mungu (swt), sio tu ni bishara njema kwetu kuhusu kuregea kwa Khilafah kwa Njia ya Utume. Hapana, Hadith hii iliyobarikiwa pia ni habari (khabar) tuifanyie kazi, kwani ni wajibu juu yetu kuhukumu kwa yale yote aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu (swt). Imepita miaka mia tangu kuvunjwa kwa Khilafah enyi Waislamu, basi fanyeni kazi ya kuiregesha!

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Musab Umair – Wilayah Pakistan**

# Serikali ya Uswidi Yawataka Waislamu Waachane na Uislamu!



Vituo vya televisheni vya Uswidi vya SVT na TV4 viliripoti mnamo Jumamosi usiku kwamba Waziri wa Usawa, Paulina Brandberg (wa Chama cha Kiliberali), anataka wafanyikazi wa mashule waripoti wasiwasi wote kwa Huduma za Jamii kuhusu wasichana kuvaa hijabu.

Waziri huyo wa Usawa alitangaza mnamo Jumamosi kwamba wafanyikazi wa shule hawana chaguo na ni lazima waripoti wasiwasi kwa Huduma za Jamii kuhusu wasichana wanaovaa hijabu, na kwamba wafanyikazi ambao hawatatii watakabiliwa na matokeo kwa kushindwa kwao kutii.

Naibu Waziri Mkuu Ebba Busch (wa chama cha Christian Democrats) aliandika kwenye jukwaa la X chini ya wiki moja iliyopita kuhusu mpango mpya ambapo alionyesha sera hiyo hiyo ya oanishaji kama ya serikali: “Idadi ya watu wanaotekeleza Uislamu nchini Uswidi na Ulaya, kama ilivyo kwa nchi za kiimla, ni kubwa mno. Hili lazima likome. Uislamu lazima ujichanganye na maadili yetu msingi ya kawaida.

Kinachomuudhi na kumkasirisha Ebba ni kwamba Waislamu nchini Uswidi wanatekeleza Uislamu, wanashikamana na kitambulisho chao cha Kiislamu na

***Endelea... UK 8***

kutekeleza ibada zake, ikiwemo kuvaa hijabu. Ebba anataka kukomeshwa kwa hili.

Hii sio habari ya kupotosha inayolenga kuharibu sifa ya Uswidi ulimwenguni. Haya ni maneno ya mawaziri wenyewe, na majaribio duni ya kusema kwamba hii ni sintofahamu hakuwadanganyi Waislamu.

Waislamu hawaamini kwamba madai ya kejeli ya Ebba Busch anafanya hivyo kwa manufaa ya Waislamu "wazuri" na kwamba anafurahia kuwa upande wao. Hii ndiyo sura halisi ya serikali ya Uswidi na hii ndiyo sera yake dhidi ya Uislamu ambayo kwayo inabeba jukumu la kimataifa!

Sera za serikali hususani hila za vyama hivi haziwawakilishi watu wa Uswidi, na hivyo hili linawapa jukumu kubwa zaidi wananchi kutangaza kuwakataa wawakilishi wao wa vyama kwa kutumia sera hizo zinazoifanya nchi ya Uswidi kuwa mbaya zaidi.

Sera ya serikali ya Uswidi ya kuwaoanisha watoto wa Kiislamu inalenga kufuta kitambulisho chao cha Kiislamu, ikiwa ni pamoja na wajibu wa kibinafsi wa Kiislamu kama vile hijabu. Serikali ya Uswidi inazidisha vita vyake dhidi ya maadili na kitambulisho cha Waislamu kwa kuharamisha hijabu na kuwateka nyara watoto kutoka kwa wazazi wao ikiwa watasisitiza kuwalea kwa mujibu wa maadili ya Kiislamu.

**Enyi Waislamu:** Kujihifadhi kibinafsi, familia ya mtu, na kudumisha kitambulisho cha Kiislamu ni wajibu wa Kisharia. Anasema Mola wetu Mlezi (swt):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَاراً وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ

**"Enyi mlio amini! Jilindeni nafsi zenu na ahali zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe."** [At-Tahrim: 6].

Tunayoyapitia sisi Waislamu ni kwa sababu sisi ni madhaifu na tunatenda kama watu waliogawanyika. Ni lazima tutende kama kundi moja, yaani, kama kundi muhimu katika jamii ambalo linachangia kwa njia chanya. Nchini Uswidi, kuna Waislamu zaidi ya milioni moja ambao wanahitajika na jamii ya Uswidi na hawawezi kuishi bila wao. Wao ni sehemu muhimu ya sekta ya usafiri, afya, elimu na kadhalika. Wanatii utaratibu wa umma katika jamii na hawaleti tishio au tatizo lolote kwa jamii, na wanakataa kutendewa hivyo. Ikiwa watatenda kama mwili mmoja, wanaweza kukomesha sera hii ya uoanishaji.

Njia ya kufikia hili si kwa kupitia uwiano, ambao una maana ya kuachana na maadili ya Kiislamu na kukumbatia maadili ya Kimagharibi au kushiriki katika mfumo wa kisekula. Mambo haya ni kinyume cha hayo, mangati ambayo baada ya muda mrefu yanapelekea Waislamu kusambaratika katika thaqafa ya Kimagharibi.

Wajibu wetu ni kujipanga kifikra na kisiasa; kifikra kwa kupitia kujenga mwamko baina ya vizazi vipya kuhusu mfumo na fahamu za Uislamu ili kuhifadhi kitambulisho cha vizazi hivi na kuzuia majaribio ya kuviingiza usekula. Katika ngazi ya kisiasa, Waislamu lazima wazingatie sera hizi kama suala la kutisha ambalo linawaathiri Waislamu wote nchini Uswidi na kutishia imani na kitambulisho chao. Upinzani wa kisiasa lazima uwakilishwe na Waislamu wanaofanya kazi kama mwili mmoja kupitia shughuli zinazoathiri rai jumla.

Tuna nguvu kubwa na tunaweza kushawishi rai jumla ya Uswidi, ambayo inapotoshwa na kutumiwa vibaya na uongozi fisadi wa kisiasa kwa uwongo na hila. Endapo tutaupa mgongo wajibu wetu, hali ya Waislamu nchini Uswidi itazidi kuwa mbaya. Anasema Mola wetu Mlezi (swt):

وَلَا يَزَالُونَ يُقَاتِلُونَكُمْ حَتَّى يَرُدُّوكُمْ عَن دِينِكُمْ إِنِ اسْتَطَاعُوا

**"Wala hawatoacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika Dini yenu kama wakiweza."** [Al-Baqara: 217]. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَلَن تَرْضَى عَنكَ الْيَهُودُ وَلَا النَّصَارَى حَتَّى تَتَّبِعَ مِلَّتَهُمْ قُلْ إِنَّ هُدَى اللهِ هُوَ الْهُدَى

**"Mayahudi hawawi radhi nawe, wala Wakristo, mpaka ufuate mila yao. Sema: Hakika uwongofu wa Mwenyezi Mungu ndio uwongofu."** [Al-Baqara: 120].

**H. 6 Rabi' I 1446**
**M. : Jumatatu, 09 Septemba 2024**

**Hizb-ut-Tahrir**
**Sweden**